

Mtu mmoja aliwahi kufanya utafiti kutaka kufahamu kwamba ni kitu gani kinawahamasisha watu wengi kufikia mafanikio yao kwa haraka zaidi kati ya marafiki na maadui.

Katika utafiti wake aligundua kwamba watu wengi alio wahoji na kuwafanyia utafiti walimwambia asilimia kuanza 50 hadi 75 ya mafanikio yao ilitokana na juhudi za maadui zao kuliko marafiki zao.

Ndio! Najua na wewe utaanza kujitafakari juu ya hapo ulipofika. Adui anamchang'o mkubwa sana kwenye safari yako kuelekea mafanikio kama utamtumia kwa usahihi.

Adui si wa kumkwepa ila ni mtaji wa kuutumia kufikia mafanikio yako.

Ni hekima ya tofauti kufahamu kwamba adui zako wanathamani kubwa kuliko marafiki zako (hata usipo kubali lakini

huu ndio uhalisia). Kumbuka watu hawakui na kuimarika katika vipindi vizuri vya maisha ila katika vipindi vya magumu na changamoto.

Jina lako litapata sifa kutokana na vile utajua kuwatumia adu zako. Watu hupunguza juhudini wanaposifiwa na kufarijiwa na wanaongeza juhudini pale ambao wanaoneshwa hawajafanya kitu.

Unaweza kulinganisha juhudini ya mtu anayetafuta hela na nyumbani hakuna chakula na yule anatafuta hela na nyumbani kuna kila kitu. Juhudi ya hawa watu wawili ni lazima itakuwa tofauti.

Changamoto huondoa maringo na kujihurumia ila zinaongeza nguvu ya upambanaji. Njaa imewahi kukooma hadi ukatamani kile chakula ulichokuwa unadai kwamba haulagi?

Kuna wakati utakosa watu wa kukuhurumia, usiogope huo ndio wakati unaukaribia ukuu wako.

Watu wengine wanapoona kuna watu wako kinyume nao huwa wanaanza kuwa na mashaka juu yao wenyewe, wanajihisi kwamba huwenda kuna mahali wamekosea au hajafanya vizuri.

Kupingwa haina maana umekosea, ondoa mashaka hayo. Unapoona kuna mtu anakupiga vita au anakushambulia tambua tatizo sio lako ila ni la huyo mtu.

Kama angelikuwa mtu wa hekima angelikuja kukaa chini pamoja na wewe na akwambie kinachomsumbuu lakini kama hajafanya hivyo tambua huyo ni mbinafsi na adui.

Ambatana na mimi katika kitabu hiki ni kupeleke kwenye safari ndani ya fikra

zako, ambayo ulikuwa hajawahi kwenda kwanza. Nikuonyeshe namna adui alivyo mtaji muhimu wa kukufikisha kwenye mafanikio yako. Ukimaliza kusoma kitabu hiki hutakuwa na mtazamo ule uliokuwa nao kwanza kuhusu adui.